# Juhudi za Vyombo vya Habari katika Kukuza na Kueneza Kiswahili Nchini Kenya

*Mosol Kandagor*

*Ikisiri*

Vyombo vya habari ni asasi muhimu sana katika kukuza na kueneza lugha yoyote ile, hasa katika enzi hii ya utandawazi. Vyombo hivyo ni kama vile idhaa za redio, televisheni na magazeti. Katika nchi ya Kenya kuna vyombo vya habari vinavyotoa huduma anuwai kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya wateja wao. Katika karne hii ya 21, vyombo vya habari vimelazimika kuhakikisha kuwa wateja wao wananufaika kutokana na huduma mbalimbali ambazo hutolewa kila kukicha. Huduma hizo hujumuisha kuwajuza, kuwafundisha, kuwaburudisha na hata kuelimisha jamii kwa namna moja au nyingine. Makala haya yanatathmini juhudi za vyombo vya habari katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya kwa kujikita katika gazeti la Taifa Leo, Idhaa za redio (Citizen na KBC), pamoja na kituo cha runinga[1] cha KBC.

## 1.0 Utangulizi

Kiswahili ni mojawapo ya lugha za Kibantu inayozungumzwa katika mataifa mengi ulimwenguni, hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki[2]. Katika ngazi za kimataifa, mataifa ya *kimagharibi*[3] na kimashariki[4] hutumia Kiswahili kwa kiwango kikubwa, kwa mfano katika taasisi za elimu, vyombo vya habari na miktadha mingine kama vile biashara na utalii.

Kabla ya kuja kwa wageni[5] katika pwani ya Afrika Mashariki, wenyeji walitumia Kiswahili kama lingua franka[6]. Kwa jinsi hiyo, waliweza kumudu shughuli zao za kibiashara, kueneza dini[7] na shughuli za kiutawala. Wageni walipowasili baadaye, walilazimika kujifunza Kiswahili ili waweze kukabiliana na shughuli zao za kikoloni kikamilifu. Ukoloni uliposhamiri, shughuli za kukisanifisha Kiswahili zilianza katika mwaka wa 1925. Baadaye kulianzishwa kamati ya Lugha ya Kimataifa katika mwaka wa 1930, ambayo ndiyo iliyohusika na usanifishaji wa Kiswahili katika Afrika Mashariki (Chirghdin na Mnyampala, 1977; Massamba, 2002; Mbaabu, 1995 na Kiango, 2002).

---

[1] runinga ni istilahi inayotumiwa zaidi nchini Kenya; nchini hujulikana zaidi televisheni.
[2] Kenya, Tanzania, Uganda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Rwanda.
[3] Marekani, Uingereza, Uropa na Ufaransa
[4] Korea na Uchina
[5] Walowezi, Wakoloni na Wamisheni
[6] Lugha sambazi iliyotumika kukidhi mahitaji ya biashara miongoni mwa wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki.
[7] Ukristo na Uislamu

Ingawa baadhi ya viongozi wa kikoloni kama vile Gavana Sir W.F Gowers walipendekeza Kiswahili kiwe lugha ya elimu na utawala na vilevile kama *lingua franka* katika ukanda wa Afrika Mashariki, Sir Daudi Chwa wa Uganda alilipinga pendekezo hilo (Kiango, 2002). Pia katika nchi ya Uganda, jamii ya Wabaganda walipinga vikali pendekezo la aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Iddi Amin Dada. Katika muda mfupi wa utawala wake, Rais Amin Dada alitambua Kiswahili kama lugha ya Taifa nchini Uganda (Mukuthuria, 2006).

Baada ya mataifa ya Afrika Mashariki kupata uhuru katika miaka ya 1960 Kiswahili kilikuzwa na kuendelezwa katika nyanja mbalimbali za kitaifa na kimataifa. Kila taifa katika Afrika Mashariki lilibuni sera zake kuhusu matumizi ya Kiswahili katika miktadha tofauti tofauti. Kenya na Tanzania kwa mfano, zilijaribu kukikuza na kukiendeleza kwa kukitumia katika biashara, elimu, siasa, utawala, mahakama, na katika vyombo vya habari. Ni kutokana na matumizi haya ndipo tunadai kuwa Kiswahili ni lugha yenye matumizi mengi hasa katika ukanda wa Afrika Mashariki. Mulokozi (2002) anadai kuwa Kiswahili bado kinaendelea kupata sifa kubwa, sio tu nchini Tanzania bali pia katika mataifa jirani na katika ngazi za kimataifa. Naye Choge (2012) anabainisha kuwa kwa sasa Kiswahili kinatumika katika mataifa mengi ulimwenguni, hasa katika masuala ya kiakademia, utawala na biashara. Pia, anadai kuwa kimepiga hatua kubwa sana kimatumizi kikilinganishwa na lugha nyingine za Kiafrika.

Katika mkabala huo, tunaweza kudai kuwa, Kiswahili kimepata sifa za kimataifa kwa jinsi kinavyozidi kukua na kuenea kila kukicha. Kwa jinsi hiyo, kuna haja ya kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuzwa, kinaimarishwa na kuenezwa na taasisi muhimu kama vile vyombo vya habari, hasa kupitia matangazo ya biashara, taarifa ya habari na vipindi teule vinavyopeperushwa kila siku.

Nchini Kenya Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi. Mtaalamu wa lugha Legere (2006a, 2006b) ambaye amefanya utafiti wa kina kuhusu matumizi ya Kiswahili nchini Tanzania, anadokeza kuwa hali kama hii ni dhahiri nchini Tanzania ambapo Kiswahili hutumika kwa kiwango kikubwa katika elimu, biashara na katika shughuli zote rasmi na zisizo rasmi. Kwa sababu hiyo, Kiswahili kinapaswa kukuzwa na kuenezwa na asasi mbalimbali zinazohusika ili kiendelee kuwa lugha maarufu katika ukanda wa Afrika Mashariki, bara la Afrika na ngazi za Kimataifa.

Makala haya yanatathmini na kubainisha juhudi za vyombo vya habari katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Kenya Kwa kuchambua juhudi za

gazeti la Taifa leo, vipindi vya redio na runinga (KBC na Citizen). Katika vipindi vya runinga, tumejikita katika idhaa ya KBC pekee. Tumechagua vyombo hivyo vya habari kwa kuwa mosi vyote vinapeperusha vipindi teule kwa Kiswahili, na kwamba hujumuisha mawasiliano ya kimazungumzo, kimaandishi na kielektroniki. Sababu ya kuchagua gazeti la Taifa Leo ni kuwa ndilo gazeti la pekee la Kiswahili nchini Kenya linalowafikia takriban wananchi wote, na linaweza kusomwa na watu wa tabaka zote. Kwa upande mwingine idhaa za redio za KBC na Citizen ambazo zimeteuliwa huwafikia wananchi wengi zaidi kuliko idhaa nyingine. Utafiti huu ulifanyika kati ya Septemba 7, na Disemba 14, 2011.

## 2.0 Vyombo vya Habari na Lugha

Vyombo vya habari vina nafasi muhimu sana katika kukuza na kuendeleza lugha katika jamii yoyote ile. Vilevile vyombo hivyo hujizatiti kutumia lugha teule inayoeleweka kwa hadhira lengwa. Kwa jinsi hiyo, lugha husika hukuzwa na kuendelezwa kwa kiwango kikubwa (Sterling na Kittross, 1999, Williams; 1993). Kwa mujibu wa Mathooko (2006) na Kawoya na Makokha (2009), vyombo vya habari vina jukumu maalumu la kukuza na kuendeleza isimu na fasihi ya lugha yoyote ile. Katika taifa la Kenya, vyombo vya habari vimejaribu kutekeleza wajibu huu, kwa namna ambavyo huandaa na kupeperusha vipindi maalumu vinavyonuiwa kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili.

Howard (2002); Kutol, Kandagor, na Somotwo (2009) wanadai kuwa dhima kuu ya vyombo vya habari ni kutoa huduma kwa jamii. Huduma hizo ni kama vile kuifahamisha na kuihamasisha jamii kuhusiana na matukio mbalimbali yanayojiri kila siku. Katika mkabala huo, vyombo hivyo hujaribu kutumia lugha husika ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano kwa wanajamii wanaolengwa. Kwa kiasi kikubwa, vyombo vya habari hujaribu kutumia lugha sanifu ili kuhakikisha kuwa matumizi yake yanakuzwa kwa kuzingatia kanuni zake za kisarufi na fasihi vilevile. Hata hivyo, vyombo vingine vya habari hukiuka kaida za sarufi za lugha husika ili kuwafikia watu wa kizazi maalumu katika jamii, kwa mfano matumizi ya Sheng[8] miongoni mwa vijana (Kandagor, 2011).

[8] Wanaisimu mbalimbali wamejaribu kutoa maelezo juu ya asili, chimbuko na sababu za kuibuka kwa Sheng. Kwa mujibu wa Abdulaziz na Osinde (1997) na Ogechi (2005), wanaelekea kukubaliana kuwa Sheng ilizaliwa katika mitaa yenye umaskini ya Eastlands jijini Nairobi (Kenya) katika miaka ya 1970 (karne ya 20). Kuibuka kwa Sheng kulitokana na mahitaji ya mawasiliano miongoni mwa vijana waliotofautiana katika mazingira ya uwili lugha. Nadharia tete nyingine ni kuwa Sheng iliibuliwa na vijana kama lugha ya kuhifadhi siri zao katika mitaa ya mabanda ambapo wazazi na wanao walilazimika kuishi katika vibanda vya chumba kimoja. Basi Sheng ikawa lugha ya vijana waliyoitumia kuzungumzia mambo yao pasipo wazazi wao kufahamu mawasiliano yao. Huenda Sheng ilitekeleza majukumu hayo katika miaka ya 1970; lakini kwa sasa, Sheng inazungumzwa na watu wengi takriban sehemu zote nchini Kenya hasa mijini (King'ei, 2001 na Shitemi, 2001).

Howard (2002) na Kandagor (2011) wanadai kuwa katika hali ya kawaida, vyombo vya habari hufikia hadhira kubwa na huwasilisha ujumbe wa aina tofauti tofauti kuhusu nyanja mbalimbali za maisha. Vilevile, huwafikia watu wengi kwa wakati mmoja. Vyombo vya habari vina uwezo mkubwa wa ama kuendeleza au kuharibu lugha. Kiswahili kinanufaika sana kutokana na jukumu muhimu linalotekelezwa na vyombo vya habari katika harakati za kukikuza, kukiendeleza na kukisambaza. Katika mataifa ya Afrika mashariki na kati, vyombo vya habari viko katika mstari wa mbele kukuza na kuendeleza lugha hii ambapo vipindi vya redio na televisheni vinapeperushwa kwa Kiswahili kila siku.

Vyombo vya habari ni zao la maendeleo ya sayansi na teknolojia ambalo limeathiri na kubadili mwelekeo wa jamii nyingi duniani. Katika makala yake juu ya nafasi ya vyombo vya habari katika kueneza lugha ya Kiswahili hasa katika enzi hii ya utandawazi, Shoo (2004) anadai kuwa Kiswahili kama nyenzo ya mawasiliano, kimepitia njia ndefu hadi kufikia kiwango chake cha sasa. Anaendelea kusema kuwa kuanzishwa kwa redio na magazeti ya Kiswahili, si tu kwamba kumesaidia katika kukikuza Kiswahili bali pia kumetoa mchango mkubwa katika ujenzi wa jamii mpya; yaani jamii ya wasemaji na watumiaji Kiswahili katika nyanja zote za maisha. Katika jamii ya sasa, utandawazi ni jambo lisiloepukika. Simala (2004 na 2006) anadai kuwa, kimsingi utandawazi unarejelea jumla ya maisha ya watu duniani; yaani unahusu uchumi, biashara, uhamaji wa watu na TEKNOHAMA[9].

Mwansoko (1995) anadai kwamba vyombo vya habari vina jukumu la kuwasilisha ujumbe mbalimbali kwa hadhira mbalimbali kutegemea muktadha husika. Anasisitiza kuwa mafanikio ya vyombo vya habari katika kuufikisha ujumbe kwa usahihi kwa watu hutegemea sana uelewa mzuri wa istilahi zinazohusiana na mada anuwai wanazozishughulikia waandishi na watangazaji wa habari. Kwa upande mwingine anasisitiza kuwa ujuzi na ufahamu wa lugha ni kipengele muhimu katika uandaaji na usambazaji wa habari katika vyombo vya habari.

Kwa ujumla jambo linalokubaliwa na watu wengi ni kwamba vyombo vya habari vimetoa mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza Kiswahili. Hata hivyo, ni vema kutaja kwamba, vyombo vya habari vina umuhimu na uwezo wa

---

Momanyi (2009), anaelekea kukubaliana na dai kuwa Sheng ni msimbo unaotumiwa hasa na vijana ili kuwatenga wengine katika mawasiliano yao. Anaendelea kudai kuwa mazingira yaliyochangia kuibuka kwa Sheng katika miaka ya mwanzo ni tofauti na ya sasa (karne ya 21). Anasema kuwa, awali Sheng ilizungumzwa na vijana) ambao hawakuzungumza Kiswahili sanifu, haja yao kuu ilikuwa ni kuwasiliana.

[9] Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

kuendeleza, kukwamisha au hata kupotosha lugha husika. Jambo hili linatokea hasa ikizingatiwa kwamba kuna makosa mengi yanayotokea katika matumizi ya lugha miongoni mwa watangazaji wa vipindi mbalimbali. Makosa hayo, ama yanaweza kutokea kwa makusudi au bila kutarajiwa.

Kwa mujibu wa Halliday (1985) lugha inaweza kutafitiwa katika muktadha wa matumizi yake. Katika mwelekeo huu, matatizo ya kijamii na uhusiano hujadiliwa na kusuluhishwa. Kutalii lugha ni mchakato ambao uhusisha mitagusano ya sayansi za jamii na masuala ya kiisimu yanayoibuliwa na tabia mahususi ya mtu binafsi au wanajamii. Ukuzaji na uendelezaji wa Kiswahili katika vyombo vya habari unaweza kuimarishwa kwa kusisitiza matumizi sahihi ya lugha.

Kama ilivyodokezwa hapo awali, makala haya yanatathmini nafasi ya vyombo vya habari katika kukuza na kuendeleza Kiswahili. Sehemu inayofuata inabainisha na kutathmini dhima ya vyombo vya habari katika kukuza na kuendeleza Kiswahili nchini Kenya.

## 3.0 Dhima ya Vyombo vya Habari katika Kukuza na Kueneza Kiswahili

### 3.1 Idhaa ya Redio KBC

Idhaa ya redio ya KBC[10] ni kituo cha kwanza kuanzishwa katika taifa la Kenya. Azma kuu ikiwa ni kuwafahamisha wananchi kuhusu yale yanayotendeka kila uchao ndani na nje ya nchi. Lugha zinazotumika kutoa matangazo katika idhaa ya redio ya KBC ni Kiingereza, Kiswahili na lugha mama. Makala haya yanajikita katika matangazo na vipindi vinavyoangazwa kwa Kiswahili.

Kwa miongo kadha baada ya uhuru, kituo cha KBC kimetumika kuwafahamisha Wakenya matukio mbalimbali yanayojiri kila siku. Mbali na kuwa chombo cha kuwafahamisha, idhaa hii pia imetumika kuwaelimisha wanafunzi wa shule za msingi na upili kupitia vipindi vinavyotolewa na Taasisi ya Elimu nchini Kenya (KIE[11]). Mojawapo kati ya masomo yanayofundishwa ni Kiswahili, yaani Isimu na Fasihi.

(a) Mafunzo/Masomo kwa Wanafunzi

Kipindi hiki hujulikana kama *KBC broadcast to schools*, ambacho huandaliwa na KIE na kutangazwa hewani na shirika la taifa la KBC. Taasisi hiyo huandaa mafunzo katika masomo anuwai, kama vile Bioolojia Kiingereza, Historia, Hisabati na Kiswahili. Vipindi vya Kiswahili vinavyopeperushwa ni hivi vifuatavyo:

---

[10] *Kenya Broadcasting Cooperation*

[11] *Kenya Institute of Education*

***(i) Kila Alhamisi***

| ***Kipindi*** | ***Wakati*** |
|---|---|
| Kiswahili Darasa la saba | Saa 3.50 |
| Kiswahili Lugha Kidato cha tatu | Saa 4.15 |
| Kiswahili Darasa la nne | Saa 5.30 |
| Fasihi ya Kiswahili kwa sekondari | Saa 3.20 |

***(ii) Kila Jumanne***

| ***Kipindi*** | ***Wakati*** |
|---|---|
| Kiswahili kwa Darasa la sita | Saa 3.50 |

Kwa kiasi kikubwa, vipindi hivi huchangia katika kukuza na kuendeleza Kiswahili. Mbali na kunufaika kiakademia kutokana na vipindi hivi, wanafunzi na walimu wanakuza kiwango chao cha msamiati. Kwa jinsi hiyo, idhaa ya redio ya KBC inakuza na kuendeleza Kiswahili.

### 3.2 Idhaa ya Redio Citizen

Redio Citizen humilikiwa na kampuni ya RMS[12]. Idhaa hii imekuwa ikipeperusha matangazo yake takriban mwongo mmoja uliopita. *Citizen* ni jina lenye asili yake katika Kiingereza lenye maana ya *mwananchi* katika Kiswahili. Jambo hili linaashiria kuwa ni idhaa ya kila mtu kwa kuwa husikika karibu pembe zote za Kenya na mataifa mengine pia katika ukanda wa Afrika Mashariki. Idhaa hii imechangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza na kueneza Kiswahili kwa njia zifuatazo:

#### (a) **Kipindi cha Rusha Roho**

Kipindi cha *Rusha Roho* hupeperushwa kila Jumapili kuanzia saa 10 hadi saa za jioni. Hiki ni kipindi cha muziki wa taarabu ambacho aghalabu huratibiwa na watangazaji walio na ufahamu kuhusu utamaduni wa Waswahili. Katika kipindi hiki masuala mbalimbali yanayohusu utamaduni wa Waswahili hupeperushwa.

Kupitia kipindi hiki wasikilizaji hupata fursa ya kufurahia sio tu utamu wa muziki, bali pia kujifunza msamiati wa Kiswahili. Muziki ni taaluma maalumu

[12] Royal Media Services. Pia, humiliki idhaa nyingine kama vile Ramogi FM, Chamgei FM, Inooro FM n.k.

ya sauti ambayo ni sanaa na sayansi. Ni sanaa katika utendaji na ni sayansi katika maandalizi na utendaji wake. Muziki humlazimu msanii kuwa na ubunifu wa hali ya juu na umahiri katika lugha husika. Maneno hupangwa kwa ruwaza maalumu inayozingatia urari wa vina na mizani ili kuleta mdundo unaopendeza na kuvutia.

Mbinu nyingine inayotumika katika nyimbo hizi za taarabu ni uradidi. Kuna baadhi ya maneno yanayorudiwa rudiwa, pengine kama msisitizo. Ali Hassan ni mmoja kati ya waratibu wa kipindi hiki ambaye aghalabu hufafanua na kuelezea dhana teule katika maneno maalumu katika nyimbo husika. Baadhi ya misamiati ambayo amewahi kueleza ni:

*Kikoi*: Aina ya nguo ya rangirangi ambayo huvaliwa kwa kujifunga kiunoni na hushuka mpaka miguuni
*Mbuzi*: Kifaa maalumu kinachotumika kukunia nazi
*Leso*: Aina ya kitambaa chepesi chenye maandishi kinachotumiwa na wanawake.
*Nikaha:* Sherehe ndogo ndogo ambazo huambatana na utamaduni wa Waswahili au ndoa za Kiislamu.
*Pwani*: Sehemu inayopakana na ziwa, bahari, mito.

## (b) **Bahari ya Lugha**

Kipindi cha *Bahari ya Lugha* hupeperushwa kila Jumamosi kati ya saa tatu na saa tano asubuhi. Mbali na waratibu wa vipindi ambao ni waajiriwa wa idhaa ya Redio Citizen, wataalamu[13] na mabingwa wa Kiswahili hualikwa studioni ili kusaidia katika kufundisha Kiswahili kwa Wakenya wote. Kwa upande mwingine, wasikilizaji hupewa nafasi ya kuuliza maswali kutokana na mambo waliyoyapata kwa kutumia ujumbe mfupi au kupiga simu moja kwa moja na kusikika katika televisheni zao. Kupitia kipindi hiki mambo mbalimbali kuhusu Kiswahili hasa ya msamiati, hutolewa. Baadhi ya mambo ambayo huelezwa ni pamoja na:

***(i) Msamiati wa Zaraa***

| ***Msamiati*** | ***Maana*** |
|---|---|
| Mimea kudumaa | Kutofikia hali ya kawaida |
| Kuchimba makoongo | Kuandaa mashimo ya kupandia mbegu. |
| Sia mbegu | Tia mbegu kwenye ardhi. |
| Kupalilia | Kukata au kung’oa kwekwe shambani |
| Kupogoa matawi | Kupunguza matawi ya miti au maua. |

---

[13] Walimu wa shule za upili, wahadhiri wa vyuo vikuu. Mfano: Ken Walibora na Walah bin Walah

***(ii) Msamiati wa fedha za kigeni***

| ***Msamiati*** | ***Maana*** |
|---|---|
| Dola ya Marekani | Fedha zitumiwazo Marekani |
| Randi | Fedha zitumiwazo nchini Afrika Kusini. |
| Faranga | Thamani ya fedha zitumiwazo Ufaransa, Ubelgiji, na Uswisi. |
| Naira | Thamani ya fedha zitumiwazo Nigeria |
| Pauni | Thamani ya fedha zitumiwazo Uingereza |
| Yeni | Fedha zitumiwazo Ujapani. |
| Pauni | Thamani ya fedha zitumiwazo Uingereza |
| Yeni | Fedha zitumiwazo Ujapani |

***(iii) Istilahi za Sauyansi***

| ***Kiingereza*** | ***Kiingereza*** |
|---|---|
| Earth | Dunia |
| Mercury | Zaibaki |
| Venus | Zuhura |
| Neptune | Kausi |
| Saturn | Zohali |
| Jupiter | Mushtarihi |
| Uranus | Sarteni |
| Mars | Mirihi |
| Pluto | Utaridi |

***(iv) Istilahi Nyingine***

| ***Kiingereza*** | ***Kiingereza*** |
|---|---|
| Yoghurt | Bururu tamu |
| Flask | Chupa ombwe |
| Microscope | Hadubili |
| Airtime | Muda wa maongezi |
| Avocado | Parachichi |
| Mobile phone | Rununu |

## (c) **Chemsha Bongo**

*Chemsha Bongo* ni kipindi ambacho hutokea kila Jumapili kati ya saa kumi na mbili jioni hadi saa moja usiku. Katika kipindi hiki, waratibu wa kipindi huwauliza wasikilizaji maswali kisha wanaweza kuyajibu kwa kutuma majibu yao kupitia huduma ya ujumbe mfupi au kupiga simu moja kwa moja. Baadhi ya vipengele vinavyojadiliwa ni masula ya kisiasa, ufahamu wa lugha ya Kiswahili na michezo. Mbali na waratibu wa kipindi kuuliza maswali, wasikilizaji pia hupata nafasi ya kuuliza maswali kutegemeana na mada ya siku hiyo. Hata hivyo, wakati mwingine wanaweza kuuliza maswali mengine ya jumla. Baadhi ya maswali yanayoulizwa katika kipindi hiki ni kama vile:

| ***Maswali*** | ***Majibu*** |
|---|---|
| Mtoto wa nzi anaitwaje? | Kiluwiluwi |
| Fafanua maana ya ngariba? | Anayewapasha watoto tohara |
| *Accountability* kwa Kiswahili ni nini? | Uwajibikaji |
| *Socialism* katika Kiswahili? | Ujamaa |
| *Cheetah* kwa Kiswahili? | Duma |
| Dereva wa meli anaitwaje kwa Kiswahili | Nahodha |

Kwa kiasi kikubwa vipindi vya *Rusha Roho, Bahari ya Lugha* na *Chemsha Bongo* vimechangia katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Hii ni kwa sababu vipindi hivi vinaweza kuwafikia watu wengi sana wanaoishi katika sehemu mbalimbali nchini. Aidha, kutokana na vipindi hivi, hadhira husika hukuza viwango vyao vya msamiati. Yaani, wanaweza kujifunza maneno mapya wanayoweza kuyatumia katika mawasiliano yao ya kila siku. Vilevile, watangazaji wa vipindi hivi huwachochea na kuwahimiza wasikilizaji kuyatumia maneno husika katika mawasiliano. Kwa jinsi hiyo, Kiswahili hukuzwa na kusambazwa katika sehemu mbalimbali nchini Kenya.

### 3.3 Kituo cha Runinga cha KBC

Kituo cha runinga cha KBC humilikiwa na serikali sambamba na idhaa ya redio ya KBC. Aghalabu vipindi vyote vinavyopeperushwa hewani huratibiwa na kudhibitiwa na serikali, kupitia Wizara ya Habari na Mawasiliano. Idhaa hii huandaa na kupeperusha vipindi vya Kiingereza na Kiswahili vilevile.

Baadhi ya vipindi (matangazo) vinavyopeperushwa kwa Kiswahili ni pamoja na kipindi cha *Kuna Nuru Gizani* kinachorushwa kila Jumapili kuanzia saa 1.30 asubuhi. Hiki ni kipindi kinachotoa mafundisho ya kidini. Askofu Pius Muiru huhubiri kwa Kiswahili kwa kuwa anamini kuwa ndiyo lugha inayoeleweka na kufahamika kwa Wakenya wengi. Kwa jinsi hiyo, anakuza na kueneza Kiswahili kwa kiwango kikubwa. Kipindi kingine kinaitwa *Jijenge Imani Yako*; kinarushwa kuanzia saa 3.30 asubuhi. Hiki ni kipindi kikingine kinachotoa mafunzo ya kidini kwa Kiswahili. Kama ilivyo katika kipindi cha Kuna Nuru Gizani, kipindi hiki huchangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

Pia, kila Jumatatu kuanzia saa 10.00 jioni kuna kipindi cha *Kiswahili Tukienzi*. Hiki ni kipindi ambacho kimekuwepo hewani kwa muda mrefu na hupeperushwa hewani kila Jumatatu saa kumi 10 na hukusudiwa kuwachochea na kuwahamasisha wapenzi wa matatu.

Kipo pia kipindi kiitwacho *Vitimbi*, kinachorushwa kuanzia saa 2.00 usiku. Kipindi hiki. Nia yake kuu ni kuwachangamsha na kuwaburudisha watazamaji

na wasikilizaji wake. Ingawa wahusika katika kipindi hiki huzungumza kilafudhi kutegemeana na jamii wanazoziwakilisha, kipindi hiki hukusudia kudhihirisha utaifa kupitia lugha ya Kiswahili.

Aidha, kila Jumatano kuna kipindi cha vioja Mahakamani kuanzia Saa 1.30 usiku na Mwamko mseto kuanzia saa 2.00 usiku.

Katika siku hii ya Jumatano, vipindi viwili vinavyotoa matangazo kwa Kiswahili vimetengwa kwa minajili ya kukuza na kueneza Kiswahili katika sehemu mbalimbali nchini. Kama nilivyotaja katika kipindi cha vitimbi, vioja mahakamani hukusudiwa hasa kuwaburudisha watazamaji wake. Wahusika huzungumza kwa Kiswahili chenye athari ya lugha mama. Katika kipindi cha mwamko mseto, watazamaji huburudishwa kwa nyimbo mbalimbali kutoka katika jamii mbalimbali za Kenya. Kwa kiwango kikubwa, vipindi hivyo vyote huchangia katika kukuza na kueneza Kiswahili.

Kila Alhamisi kuanzia saa 8.00 alasiri kipindi cha *Vioja Mahakamani* hurudiwa na kila Ijumaa kuanzia saa 10.10 ni ukumbi wa Kiislamu. Hiki ni kipindi kinachotoa mafunzo ya dini ya Kiislamu kwa Kiswahili. Kwa jinsi hiyo, lugha ya Kiswahili hukuzwa na kuenezwa kila siku ya kipindi hiki. Mwisho ni Kila Jumamosi ambapo vipindi luluki hupeperushwa hewani. Navyo ni :

| ***Kipindi*** | ***Wakati*** |
|---|---|
| Je, huu ni ungwana? | Saa 8.30 Alasiri |
| Dunia Wiki Hii | Saa 9.15 Alasiri |
| Kiswahili Tukienzi | Saa 11.00 Jioni |

*Je, huu ni ungwana*? ni kipindi ambacho huandaliwa na kupeperushwa hewani na mtangazaji mkongwe anayejulikana kama Leonard Mambo Mbotela. Kipindi hiki kinahusu hulka na maadili mema miongoni mwa watu mbalimbali katika jamii. *Dunia wiki hii* huangazia habari mbalimbali za ulimwengu kutoka pembe zote za dunia. Kwa upande mwingine, *Kiswahili Tukienzi* ni sehemu ya pili ya kipindi kinachopeperushwa siku ya Jumatatu saa 10 jioni. Vipindi hivi kwa pamoja ni chachu kubwa ya kukuza na kueneza Kiswahili katika jamii ya Kenya.

## 3.4 Gazeti la Taifa Leo

Hili ni gazeti linalochapishwa kila siku na shirika la NMG[14]. Ingawa gazeti hili huchapishwa ili kusomwa na Wakenya wote, ni watu wachache sana husoma. Kutokana na utafiti tulioufanya, ni bayana kuwa wasomaji wa gazeti hili wengi

[14] *Nation Media Group*

ni watu wasio na kiwango kikubwa cha elimu. Kwa kiasi kikubwa, gazeti hili limeishia kuwa la mabawabu, wazee, na kuhifadhiwa kwenye maktaba za kitaifa na taasisi za elimu. Kutokana na uchunguzi wetu, gazeti la *Taifa Leo* hutumia njia zifuatazo kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili:

(a) **Mashairi**

Wahariri wa gazeti hili huwaomba wapenzi wa mashairi kuyatuma mashairi ambayo yanaweza kuchapishwa. Ingawa watu wengi huyatuma mashairi ili yachapishwe katika gazeti la *Taifa Leo*, wengi wao ni wananchi wa kawaida ambao wanapenda Kiswahili, na wala sio wanataaluma. Wanataaluma wa Kiswahili, hasa walimu na wanafunzi, hutuma mashairi kwa kiwango kidogo sana. Mfano wa mashairi yaliyowahi kuchapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* ni haya yafuatayo:

Anwani: ***Namwamini***
Ubeti wa 1: Nimetia tuli, yenu nyie sikia
Mwisho meona muhali, uwanjani kutokeza,
Niueleze ukweli, kujua mupate weza,
Mungazidisha majungu, ndoa hamtaivunja
Shairi la Khamis Darwesh: Agosti 30, 2009

Mbali na mashairi yanayochapishwa tu kwa ajili ya kusomwa na watu mbalimbali, kuna sehemu nyingine inayohusu uchambuzi wa mashairi. Sehemu hii inanuiwa kuwasaidia hasa wanafunzi wa taasisi tofauti tofauti za elimu kudurusu wanapojiandaa kufanya mtihani wa kitaifa, yaani K.C.P.E[15] au K.C.S.E[16].

Anwani: ***Sitonena Tena***
Ubeti wa 1: Kwi kwi kwi Tim nalia, nalia wangu mpendwa
Andanje nina mlia, manya kazi wa hodwa
Shiraha wana mlia, mwana wakwao mpendwa
Andanje mlaze pema, ilhali mola Karima

Shairi la Timothy Chitui Mollah: Julai 13, 2009

*Swali*: Shairi hili latupa ujumbe gani? (Alama 3)
*Jibu*: Latuonyesha hisia za Wakenya kuhusu wale waliosababisha ghasia za baada ya uchaguzi mkuu wa 2007.

Hii ni baadhi ya mifano ya mashairi yanayochapishwa na gazeti hili na kusaidia kukuza na kueneza Kiswahili na fasihi yake.

---

[15] *Kenya Certificate of Primary Education*
[16] *Kenya Certificate of Secondary Education*

(b) **Istilahi za Biashara na Matangazo ya biashara**

Gazeti la *Taifa Leo* hutenga nafasi ya istilahi za biashara na pia matangazo ya biashara. Sehemu hii ni chachu kubwa katika kukuza na kueneza Kiswahili. Mfano mzuri hapa ni tangazo la biashara la Shirika la Safaricom:

> Hujawahi tuma barua pepe?
> Anza kutuma Ovi Mail kupitia simu yako ya Nokia
> Tuma na pokea barua pepe wakati wowote,
> Pahali popote moja kwa moja kwa simu yako…..

Katika tangazo hili, baadhi ya wasomaji wanaweza kujifunza istilahi mpya kama vile *barua pepe*. Ingawa maana ya istilahi hii haijatolewa katika tangazo hili, wasomaji wanaweza kunukuu na kuuliza kupata maana yake. Kimsingi *barua pepe* ni istilahi inayorejelea barua au waraka unaoandikwa na kutumwa kupitia mtandao wa intaneti. Pia, ni nadra sana kupata tangazo la biashara lililoandikwa kwa lugha ya Kiswahili katika magazeti. Matangazo mengi ya biashara nchini Kenya hutolewa kwa lugha ya Kiingereza kupitia magazeti kama vile *The Standard, The Star* na *Nation*. Kwa jinsi hiyo, gazeti la *Taifa Leo* limepiga hatua kubwa katika kukuza na kueneza Kiswahili kupitia matangazo ya biashara.

Pia, katika ukurasa wa 21, wahariri huchapisha istilahi zinazohusu ubadilishaji wa fedha za kigeni, bei za bidhaa na utendaji kazi wa benki.Tazama mifano ifuatayo:

Bidhaa Sokoni

***Mazao***
Mahindi makavu
Maembe
Ndizi Mbivu
Ngano
Mwitenamia
Malimau
Njugu
Mahindi Mabichi
Vitunguu
Sukuma wiki (Agosti 5, 2009)

(iii) Ubadilishaji wa fedha*:*

**Sarafu**
Dola ya Marekani
Pauni ya Uingereza
Euro ya Ulaya
Randi ya Afrika Kusini
Shilingi ya Kenya
Franka ya Uswizi
Rupia ya India
Dola ya Hong Kong (Julai 31, 2009)

Kama ilivyokuwa katika mfano wa tangazo la safaricom istilahi za bei za bidhaa (mazao) na ubadilishaji wa fedha (sarafu) ni juhudi nyingine muhimu inayotekelezwa na wahariri wa gazeti la *Taifa Leo* katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Wasomaji basi wanaweza kujifunza istilahi mpya zinazorejelea mazao na sarafu.

(b) **Vitendawili**

Gazeti la *Taifa Leo* huwa na sehemu ya vitendawili. Katika sehemu hiyo, maswali ya vitendawili huulizwa. Maswali hayo huandamana na majibu ambayo hutolewa kwingineko katika ukurasa huo huo.

| ***Kitendawili*** | ***Jibu lake*** |
|---|---|
| Wafu wanakokotana | Jahazi na Tanga. |
| Ghala lake limejaa punje za mahindi | Kinywa |
| Kaka ana jicho moja | Sindano |
| Shamba langu lina miti miwili tu | Masikio |
| Atolewapo nje hufa | Samaki |
| Chemba huwa kito | Lulu |
| Gari la bwana Ali halitumii mafuta | Miguu ya binadamu |
| Inama nikwambie | Mwiba |
| Ulimi wa kulazia | Udanganyifu kwa kutumia maneno matamu. |

Mfano wa Vitendawili Julai na Agosti 2009

Katika sehemu hii, lengo kuu ni kuwachangamsha wasomaji wake. Mbali na kuwaburudisha wasomaji, vitendawili vinaweza kuwachochea wasomaji kupenda lugha ya Kiswahili. Kwa kweli hii ni juhudi mojawapo inayooneshwa na gazeti la *Taifa leo* katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya.

(d) **Methali**

Katika sehemu hii, wahariri hutenga ukurasa maalumu ambapo wasomaji huweza kuburudika kwa kusoma na kukamilisha methali. Msomaji huhitajika kutoa jibu kwa methali kutegemeana na jinsi swali lilivyoulizwa. Tazama mifano ifuatayo:

| *Maswali* | *Majibu* |
|---|---|
| Hapana raha isiyo | karaha |
| Lililopo ndilo | lisemwalo |
| Jiwe moja | halinjiki chungu |
| Macho ya chura hayamnyimi | ng'ombe kunywa maji |
| Mchelea mwana kulia | hulia yeye |
| Mchakato ujao haulengwi | na jiwe |
| ……….akisifiwa tembo hulitia maji | Mgema |
| ……….ni mali kila mtu ana zake | Akili |
| ……….haiji ila kwa njia ya upanga | Amani |
| Hakika kama | mauti. |
| Apigaye mbinja | mwishowe ataimba. |

(Julai na Agosti, 2010)

### (e) **Tashbihi**

Kama ilivyo katika methali na vitendawili wasomaji pia huburudishwa na wahariri wa gazeti la *Taifa Leo* kwa maswali ya tashbihi, ambapo hadhira husika inatarajiwa kuyajibu. Majibu hufichwa sehemu fulani katika ukurasa huo huo.

| *Maswali* | *Majibu* |
|---|---|
| Nyanyasa kama | mbwa |
| Nyoofu kama | kondoo |
| ……….kama ambari na zindua/ kumbikumbi/mapacha | Pendana |
| Shingo kama ya | mbuni |
| ……….kama jibwa lisilo kwao/mbwa koko | Zurura |
| Washa kama | upupu |
| Zima kama | barafu |
| Tegemeana kama pua na | mdomo |
| Rundika kama | magunia |
| Pepesuka kama | mlevi |

(Julai 30, 2009)

Katika sehemu ya methali na tashbihi madhumuni hasa ya maswali yanayoulizwa na majibu yanayotolewa kwa maswali husika, ni kuwachochea wasomaji wa gazeti la *Taifa Leo* kukipenda Kiswahili na hivyo basi kuikuza na kukieneza. Wasomaji wengi wa methali na tashbihi hizo hununua gazeti hilo ili kujifunza methali na tashbihi mpya na pia kuelimika na kujiburudisha. Mbali na kuburudika, wasomaji husika huibuka kuwa wapenzi wa Kiswahili.

### (f) **Chemsha Bongo**

Katika sehemu hii maswali hurejelea mambo au vitu vya kijumla jumla. Maswali haya huandaliwa na wahariri wa gazeti hilo la Kiswahili. Wasomaji hutarajiwa kuyasoma maswali yale na kisha kutoa majibu mwafaka. Tazama mifano ifuatayo:

| ***Maswali*** | ***Majibu*** |
|---|---|
| Kituo cha redio cha QFM kinamilikiwa na kampuni gani | Nation Media Group |
| Kinuthia Mbugua anasimamia kitengo kipi cha polisi? | Utawala |
| Shrika la CNN linamilikiwa na Mkenya, ni kweli au uwongo? | Uwongo |
| Mataifa matano wanachama wa UN wenye kura ya turufu ni yapi? | ? Uchina, Marekani, Urusi,<br><br>Uingereza na Ufaranza |
| Kilwa ni kisiwa kilicho kusini mwa nchi gani Afrika Mashariki? | Tanzania |
| Garishon Kirima ni mbunge wa zamani wa eneo linalowakilishwa<br>na nani sasa? | Askofu Margaret Wanjiru |

(Imenukuliwa katika magazeti ya Julai na Agosti, 2009/2011)

Maswali yanayoulizwa katika sehemu ya *chemsha bongo* yanalenga hasa kuwachangamsha wasomaji mbalimbali wa gazeti la *Taifa Leo*. Hata hivyo, kwa kuwa maswali haya huulizwa kwa lugha ya Kiswahili, wasomaji wake hatimaye huwa wapenzi wa lugha hiyo. Hivyo basi, gazeti hilo litakuwa limetekeleza kazi ya kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya.

## 4.0 Hitimisho

Makala haya yametathmini nafasi na juhudi za vyombo vya habari katika kukuza na kueneza Kiswahili. Kutokana na makala za gazeti la *Taifa Leo* na vipindi vyote katika idhaa (KBC na Citizen) tulizorejelea, imebainika kwamba vyombo vya habari hutekeleza jukumu muhimu sana katika kukuza na kuendeleza Kiswahili kwa kiwango kikubwa. Vyombo hivyo vya habari si asasi muhimu tu katika harakati za kukuza, kueneza na kuimarisha Kiswahili, bali pia ni taasisi zinazoweza kutegemewa na kuthaminika katika jitihada zake. Ili kuimarisha na kudumisha juhudi zinazotekelezwa na vyombo vya habari katika harakati za kukuza na kueneza Kiswahili, serikali ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba kuna sera maalumu inayodhibiti matangazo ya vipindi vinavyopeperushwa na vituo mbalimbali vya habari nchini. Serikali inaweza kutunga sheria itakayohakikisha kuwa kila kituo cha habari angalau kiwe na vipindi zaidi ya kimoja vinavyokusudiwa kuimarisha na kudumisha lugha ya Kiswahili, hasa ikizingatiwa kuwa lugha hii si ya kitaifa tu, bali pia ni rasmi nchini Kenya. Pia, waandaji wa vipindi vya Kiswahili wanaweza kuwahusisha wataalamu wa lugha ili sarufi na vipengele vingine vya kimsingi katika lugha visivurugwe.

Kwa upande wa magazeti, kuna haja ya kuimarisha gazeti la *Taifa Leo* kwa kuhakikisha kuwa usomaji wake unapanuliwa, ili lisionekane kuwa ni la mabawabu na wengine wasiofahamu Kiingereza vizuri. Wataalamu wa Kiswahili wanapaswa kulisoma pia ili waweze kupendekeza namna ya kuliimarisha zaidi kwa minajili ya kukuza na kueneza Kiswahili. Kwa vyovyote vile, vyombo vya habari vinahitaji pongezi kubwa kwa juhudi zake za kukuza, kueneza na kuimarisha Kiswahili, sio tu nchini Kenya bali pia katika ukanda wa Afrika Mashariki, Afrika na hata kimataifa.

## Marejeo

Abdulaziz, M.H. na K. (Osinde, 1997). “Sheng and English: Development of A Codes Mixed Among Urban Youth in Kenya.” *International Journal of the Sociology of Language*. Berlin.

Chirghdin, S. na M. Mnyampala, (1977). *Historia ya Kiswahili*. OUP, Dar-es-Salaam.

Choge, S. C. (2012). “Fifty Years of Kiswahili in Regional and International Development.” *Journal of Pan African Studies*. Juz. l. 4, Na. 10, 172-203.

Cowie, A.P na wenzie (1992). *Oxford Advanced Learner’s Dictionary*. OUP.

Halliday, M.A.K. (1985). *Explorations in the Functions of Language*. N.Y: Edward.

Howard, R. (2002). “An Operational Framework for Media and Peace Building**.**

Kandagor, M.M. (2011). Uchanganuzi wa Jumbe Fupi katika Mawasiliano ya Rununu: Mtazamo wa Kisajili.” Tasnifu ya Uzamifu, Chuo kikuu cha Moi.

Kiango, J. G (2002). “Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki”. *Swahili Forum*. IX. 143-154.

King’ei, K. (2001). “Language and Identity: The Challenge of Sheng in Kenya.” *Association of Third World Studies Conference*, Septemba 17-19. Chuo Kikuu cha Egerton.

Kowoya, V na J. Makhoha, (2009). “The Case for Kiswahili as a Regional Broadcasting Language in East Africa.” *Journal of Pan African Studies*. Vol 2. No. 8. 11-35.

Kutol, K, M. Kandagor, na P. Simotwo. (2009). “The Role of Media in 2007 Post-Election Violence: The Case of Standard and Taifa Leo Newspapers.” *Journal of Intra African Studies* Juz. 2. 24-43.

Legere, K. (2006a). “Swahili’s Current Spread to a Remote Area: Data from primary schools in Vidunda Ward (Central Tanzania).” *Africa in the Long Run*. 93-109. Helsinki: Finnish Oriental Society.

Legere, K. (2006b). *“Formal and Informal Development of the Swahili Language: Focus on Tanzania.” Selected Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistics*. 176-184. Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project.

Massamba, D.P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: JKF.

Mathooko, P.M. (2006). “Fasihi Simulizi: Chombo Hifadhi cha Lugha za Kiafrika.” *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. 41-46.

Mbaabu, I. (1995). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Longman: Nairobi.

Momanyi, C. (2009). “The Effects of sheng in the Teaching of Kiswahili in Kenyan Schools.” *Journal of Pan African Studies,* Juz. 2 Na. 8; 127-138

Mukuthuria, M. (2006). "Kiswahili and its Expanding Roles of Development in East African Cooperation: A Case of Uganda." *Nordic Journal of African Studies.* 15 (2): 334-355.

Mulokozi, M. M. (2002). "Kiswahili as National and International Language." Institute of Kiswahili Research. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Mwansoko, H.J.M. (1995). "Dhima ya Vyombo vya Habari katika Ukuzaji, Usanifishaji na Uenazaji wa Istilahi." *Kiswahili katika Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam: TUKI.

Ogechi, N. O. (2005). "On Lexicalization in Sheng." *Nordic Journal of African Studies.* 14 (3): 334-355.

Posteguillo, S. (2003). *Net Linguistics*: *Language, Discourse and Ideology in Internet*.

Shitemi, N. L. (2001). "Pidginization Sheng, the melting-pot of the Kenyan languages and anti-Babel development." Katika *Kiswahili*: *Journal of the Institute of Kiswahili Research* Juz. 64:1-16

Shoo, G. (2004). "Nafasi ya Kiswahili katika Vyombo vya Habari wakati huu wa Utandawazi." *Kiswahili na Utandawazi*. Dar es Salaam: BAKITA 79-86.

Simala, K. I. (2004). Uzalendo wa lugha ya Kiswahili katika enzi ya Utandawazi. Kiswahili na Utandawazi. BAKITA. Dar es Salaam. 34-44.

Simala, K. I. (2006). *Fasihi Simulizi katika enzi ya Utandawazi*. Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Twaweza Communications.

Sterling, C. and J. Kittross. (1990). *The age of Television. In Stay Tuned: A Concise History of American Broadcasting*. Belmont, CA: Wadsworth.

Williams, K. (1993). "The Light at the end of the Tunnel: The Mass Media, Public Opinion and the Vietnam War." katika G*etting the Message: News, truth and power*. London.